**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA MWAKA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 19/07/2022 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA SOKO KUU LA CHIFU KINGALU.**

**Wajumbe waliohudhuria**:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pascal M. Kihanga | __ | Mstahiki Meya – Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Ally H. Machela | __ | Mkurugenzi wa Manispaa -Katibu |
| 3. | Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele | __ | Naibu Meya - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah | __ | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Aisha Ahmad Kitime | __ | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Grace Luwis Mkumbae | __ | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Latifa Saidi Ganzel | __ | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani | __ | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Marco Mathias Kanga | __ | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Melchior Peter Mwamnyanyi | __ | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Salum Mrisho Chunga | __ | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu | __ | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Warda Omari Bazia | __ | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Rahma Lashayo Maumba | __ | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Amini Abdallah Tunda | __ | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mwanaidi Ebrahim Ngulungu | __ | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma ( Mb) | __ | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | __ | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Juma Issa Kiduka | __ | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Samuel Alfred Msuya | __ | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Zuberi George Mkalaboko | __ | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Madaraka S. Bidyanguze | __ | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Selestini Savini Mbilinyi | __ | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Rashid Ramadhani Matessa | __ | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Hadija Kombo Kibati | __ | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Mch. Thomas Benedict Butabile | __ | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Peter Joel Dhahabu | __ | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Lt.Col.(Mst) Ahmed S. Mazora | __ | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Salima Bonzo Mbandu | __ | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Abdallah Ally Meya | __ | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Joel Albert Kisome | __ | Mjumbe |
| 32. | Mhe. Hamisi Ally Kilongo | __ | Mjumbe |
| 33. | Mhe. Amina Hussein Zihuye | __ | Mjumbe |
| 34. | Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu | __ | Mjumbe |
| 35. | Mhe. Seif Zahoro Chomoka | __ | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 36. | Mhe. Namala Johaness Mchunguzi | __ | Mjumbe |
| 37. | Mhe. Zinduna Kombo Selemani | __ | Mjumbe |
| 38. | Mhe. Athumani Omary Lujuo | __ | Mjumbe |
| 39. | Mhe. Eng. Hamisi Hamad Ndwata | __ | Mjumbe |

**Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb) | __ | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Norah Mzeru (Mb) | __ | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Emmy Kiula Rajabu | __ | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hassan Madadi Maringo | __ | Mjumbe |

**Viongozi waalikwa waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Chief Sylvester Yaredi | __ | Katibu wa CCM Wilaya |
| 2. | Mhe. Fikiri Juma | __ | Mwenyekiti wa CCM Wilaya |
| 3. | Mhe. Maulidi Chambilila | __ | Katibu Mwenezi na Siasa CCM Wilaya |
| 4. | Ndg. Hilary B. Sagara | __ | Kaimu Katibu Tawala Wilaya |

**Wakuu wa Idara na Vitengo waliohudhuria;**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Pilly R. Kitwana | __ | Afisa Utumishi wa Manispaa |
| 2. | Ndg. Neema Michael Dachi | __ | Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa |
| 3. | Ndg. Epiphania Matafu | __ | Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa |
| 4. | Ndg. Josephine Mkuli | __ | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa |
| 5. | Ndg. Winfred A. Kipako | __ | Afisa Tarafa Manispaa |
| 6. | Ndg. Gabriel Paul | __ | Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa |
| 7. | Ndg. Chausiku Masegenya | __ | Afisa Elimu Msingi  wa Manispaa |
| 8. | Dr. Tito Kagize | __ | Afisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Manispaa |
| 9. | Ndg. Samwel Subi | __ | Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu wa Manispaa |
| 10. | Ndg. Upendo Elias | __ | Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa |
| 11. | Eng. Juma Gwisu | __ | Kaimu Afisa Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mijini wa Manispaa |
| 12. | Ndg. Feliciana Katemana | __ | Mratibu wa TASAF wa Manispaa |
| 13. | Ndg. Elikarim S. Tyeah | __ | Kaimu Mwanasheria wa Manispaa |
| 14. | Ndg. Isaac Ashery | __ | Kaimu Mweka Hazina wa Manispaa |
| 15. | Ndg. Evance Kutona | __ | Afisa Usafirishaji wa Manispaa |
| 16. | Ndg. Festus Herman | __ | Afisa Viwanda, Biashara na Uwekezaji wa Manispaa |
| 17. | Ndg. Sophia Kingwahi | __ | Afisa Michezo, Utamaduni na Sanaa wa Manispaa |
| 18. | Ndg. Jafari A. Makupula | __ | Afisa Ununuzi na Ugavi wa Manispaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 19. | Ndg. Kitutu Mshana | __ | Afisa Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu wa Manispaa |
| 20. | Ndg. Adam T. Shayo | __ | Mthibiti Ubora wa Shule Wilaya |
| 21. | Ndg. Kelvin A. Chale | __ | Kaimu Katibu TSC Manispaa |
| 22. | Ndg. Norbert Bilaba | __ | Afisa Afya wa Manispaa |
| 23. | Ndg. Jeremiah Lubereje | __ | Afisa Mipango na Uratibu wa Manispaa |
| 24. | Dr. Felista Stanslaus | __ | Kaimu Mkuu wa Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Manispaa |
| 25. | Ndg. Alatutosia Y. Sanga | __ | Afisa Masoko |
| 26. | Ndg.Lilian Henerico | __ | Afisa Mawasiliano wa Manispaa |

**Watendaji wa Kata waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg Asha Mziray | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Lukobe |
| 2. | Ndg. Baraka Lemaha | __ | Mtendaji wa Kata ya Mindu |
| 3. | Ndg. Hadija K. Hamisi | __ | Mtendaji wa Kata ya Mji Mkuu |
| 4. | Ndg. Mwajabu R. Hassani | __ | Mtendaji wa Kata ya Mafisa |
| 5. | Ndg. Merina C. Singano | __ | Mtendaji wa Kata ya Kichangani |
| 6. | Ndg. Jafery Azizi Habibu | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Mkundi |
| 7. | Ndg. Amina Said | __ | Mtendaji wa Kata ya Mafiga |
| 8. | Ndg. Josepher B. Kisaka | __ | Mtendaji wa Kata ya Kihonda Maghorofani |
| 9. | Ndg. Mariam Khalid Ngoda | __ | Mtendaji wa Kata ya Uwanja wa Taifa |
| 10. | Ndg. Helena W. Mgallah | __ | Mtendaji wa Kata ya Bigwa |
| 11. | Ndg. Hendrica A. Lokilo | __ | Mtendaji wa Kata ya Mlimani |
| 12. | Ndg. Bright Sospeter | __ | Mtendaji wa Kata ya Kilakala |
| 13. | Ndg. Ibrahim R. Nguya | __ | Mtendaji wa Kata ya Kingolwira |
| 14. | Ndg. Witness Matowo | __ | Mtendaji wa Kata ya Magadu |
| 15. | Ndg. Mariam s. Rajabu | __ | Mtendaji wa Kata ya Mbuyuni |
| 16. | Ndg. Maria J. Shine | __ | Mtendaji wa Kata ya Kingo |
| 17. | Ndg. Laurent Masanja | __ | Mtendaji wa Kata ya Tungi |
| 18. | Ndg. Maria Mwangumu | __ | Mtendaji wa Kata ya Mwembesongo |
| 19. | Ndg. Prisca Mawallah | __ | Mtendaji wa Kata ya Boma |
| 20. | Ndg. Rajabu Wanyamale | __ | Mtendaji wa Kata ya Chamwino |
| 21. | Ndg. Andrew Edward Luka | __ | Mtendaji wa Kata ya Mjimpya |
| 22. | Ndg. Aziza Omari | __ | Mtendaji wa Kata ya Kiwanja cha Ndege |
| 23. | Ndg. Christina Ngonyani | __ | Mtendaji wa Kata ya Mzinga |
| 24. | Ndg. Hawa R. Uvilla | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Sultan Area |
| 25. | Ndg. Fatma H. Mkwenda | __ | Mtendaji wa Kata ya Sabasaba |
| 26. | Ndg. Masanja M. Nkinga | __ | Mtendaji wa Kata ya Mazimbu |
| 27. | Ndg. Tatu H. Ally | __ | Mtendaji wa Kata ya Kihonda |
| 28. | Ndg. John Joseph | __ | Mtendaji wa Kata ya Luhungo |
| 29. | Ndg. Jennifer S. Rashid | __ | Mtendaji wa Kata ya Kauzeni |

**Sekretarieti:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Daudi A. Kibwana | __ | Katibu wa Mikutano |
| 2. | Ndg. Deogratias Butabile | __ | Katibu wa Mikutano |
| 3. | Ndg. Theresia Mbena | __ | Katibu wa Mikutano |
| 4. | Ndg. Jimmy Katabaruki | __ | Katibu wa Mikutano |
| 5. | Ndg. Mwasi Mulwambo | __ | Katibu wa Mikutano |
| 6. | Ndg. Lilian Lemunge | __ | Katibu wa Mikutano |

HMM/BM/1/ 2022/2023 Kufungua Mkutano

Kabla ya kufungua Mkutano wajumbe waliimba wimbo wa Taifa na Dua ya kuiombea Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Baada ya Dua Mstahiki Meya alifungua Mkutano saa 4:25 asubuhi kwa kusoma hotuba ya utendaji kazi ya Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Katika hotuba hiiyo Mstahiki Meya alieleza mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hicho kama ifuatavyo.

**1.0 MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI KWA MWAKA 2021/2022**

**Mapato**

Hadi mwezi Mei, 2022 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilipokea na kukusanya fedha jumla ya **Tshs. 65,971,085,426.87** ambayo ni sawa na asilimia **83.4** ya makadirio ya **Tsh. 74,628,889,213** ya mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo:-

- Mapato ya Ndani (Own Source) yalikuwa ni **Tshs. 8,809,042,273.90** ambayo ni sawa na asilimia **85.89** ya makisio ya **Tshs.10,255,736,199.95** ya mwaka 2021/2022.

- Miradi ya maendeleo, jumla ya **Tshs.6,281,546,536.16** zilipokelewa kutoka Serikali Kuu ambazo ni sawa na asilimia **59.80** ya makisio ya **Tshs 10,504,306,600.00** ya mwaka 2021/2022.

- Mishahara jumla ya **Tshs 49,779,504,700.00** zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia **94.56** ya makisio ya **Tshs.52,640,840,813.44**

**Mikakati ya kufikia malengo**

Halmashauri ina mikakati mbalimbali ya kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

- Kutoa elimu kwa walipa kodi juu ya umuhimu wa kulipa kodi na ushuru kwa ustawi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.
- Kuwa na kikosi kazi maalum cha ufuatiliaji wa mapato ambacho kilianza katika eneo la Msamvu na sasa kinaendelea katika vyanzo vingine
- Kutoa elimu kuhusu ulipaji wa kodi mbalimbali kwa wakati kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa Manispaa ya Morogoro.

## 1.2 Matumizi

Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipanga kutumia kiasi cha **Tshs. 74,628,889,213.00** kwa matumizi mbalimbali ikiwemo mishahara, matumizi ya ruzuku, matumizi yasiyo ya ruzuku pamoja na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Mei, 2022 Halmashauri ilitumia kiasi cha **Tshs**. **59,675,356,051.52** sawa na asilimia **83.83** kwa mchanganuo ufuatao:-

- Mishahara, matumizi ya ruzuku na matumizi yasiyo ya ruzuku Halmashauri ilitumia kiasi cha **Tshs. 53,762,456,648.88** kati ya **Tshs. 64,127,584,534.80** sawa na asilimia **90.10** ya makisio.
- Miradi ya maendeleo. Halmashauri ilitumia kiasi **Tshs. 5,912,899,402.64** kati ya **Tshs, 10,504,306,600.00** sawa na asilimia **56.29** ya makisio.

## 2.0 KUHUSU SEKTA YA UCHUMI NA UWEKEZAJI:

Halmashauri imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali kwa mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo:-

## A. MIRADI ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA SERIKALI KUU.

### i) Sekta ya Elimu Sekondari

- Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2021/22 ilipokea fedha za Mpango wa Maendeleo ya **UVIKO 19** jumla ya **Tshs. 1,720,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **86** ya sekondari pamoja na viti **4,300** na meza **4,300** kwa shule **21** za serikali ikiwa **17** ni shule zilizokuwepo na **4** zimejengwa mpya. Madarasa **86** pamoja na viti **4,300** na meza **4,300** vilikamilika katika muda uliokuwa umetolewa na Serikali. Manispaa kwa kuangalia mtawanyiko wa maeneo yake ya kiutawala na ufaulu iliweza kuanzisha ujenzi wa shule mpya **4** za Mazimbu, Tungi, Mbuyuni na Mkundi. Mradi huu umeweza kuhakikisha wanafunzi **4,300** wa kidato cha kwanza kupata nafasi ya masomo bila adha yoyote.

- Manispaa ya Morogoro kupitia fedha za mradi kutoka Serikali Kuu (SEQUIP) Chini ya uongozi wa Awamu ya sita imepokea kiasi cha **Tshs. 940,000,000.00** kati ya **1,200,000,000.00** zilizopo kwenye Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya nyingine **2** za Mindu na Lukobe kwa lengo la kuboresha miundombinu ya Elimu Sekondari ndani ya Manispaa ambapo ujenzi wa vyumba **16** vya madarasa, maabara **6,** maktaba **2,** vyumba **2** vya TEHAMA, majengo **2** ya utawala na vyoo matundu **40** na ujenzi unaendelea vizuri ukiwa hatua ya upauaji.

- Manispaa ya Morogoro pia imepokea jumla ya **Tshs 100,000,000.00** kwa ajili ya umaliziaji wa maabara **4** za Sayansi kwa mgao wa **Tshs 25,000,000.00** kwa kila maabara. Maabara hizo zipo katika hatua mbalimbali za umaliziaji.

### ii) SEKTA YA ELIMU YA MSINGI

Manispaa ya Morogoro ilipokea fedha za Mpango wa maendeleo ya UVIKO 19 jumla ya **Tshs 80,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja la watoto **80** wenye mahitaji maalum. Ujenzi upo hatua za umaliziaji na umefanyika katika shule ya Msingi Norto iliyopo Kihonda.

### iii) SEKTA YA BIASHARA

Manispaa ya Morogoro imeanza kutekeleza mpango wa kuwatoa machinga barabarani kwa kuwajengea vibanda vya biashara katika maeneo mbalimbali. Jumla ya vibanda **880** vimejengwa katika eneo la Soko Kuu la Chifu Kingalu. Aidha, Manispaa imeanza ujenzi wa vibanda **546** katika maeneo ya Fire, Mtaa Mfupi, Masika na Stendi ya Mazimbu ambapo Manispaa imetumia **Tshs. 234,000,000.00** fedha za mapato ya ndani kujenga miundombinu hiyo**.** Aidha, Serikali ya awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa Tshs. **490,000,000.00** kwa ajili ya kujenga miundombinu ya biashara za Wamachinga**.**

### iv) SEKTA YA AFYA

#### a) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

Manispaa ilipokea jumla ya **Tshs 500,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa majengo **2** ya OPD na Maabara pamoja na kichomea taka. Majengo yote yamepauliwa na yapo kwenye hatua za umaliziaji.

#### b) Ujenzi wa Kituo cha Afya – Lukobe

Manispaa ilipokea jumla ya **Tshs 500,000,000.00** za ujenzi wa kituo cha Afya Lukobe kwa awamu ya mbili tofauti. Awamu ya kwanza **250,000,000.00** na awamu ya pili **250,000,000.00.** Majengo yote ya awamu ya kwanza yapo hatua za umaliziaji na kwa fedha za awamu ya pili ujenzi unaendelea.

**v) SEKTA YA MIPANGO MIJI, ARDHI NA MALIASILI**

Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilipokea mkopo wa jumla ya **Tshs. 1,000,000,000.00** kutoka Wizara ya Ardhi , Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupima ekari **4,500** baada ya wataalamu kuandika andiko la mradi wa upimaji wa ardhi. Aidha Serikali ya awamu ya sita imewezesha kupata fedha hizo na Halmashauri ya Manispaa itajitahidi kadri iwezekanavyo kuhakikisha kuwa shughuli hii ya upimaji inakamilika kama ilivyopangwa.

## B. MIRADI ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI.

### i) SEKTA YA ELIMU YA SEKONDARI

Manispaa ya Morogoro kupitia fedha za mapato ya ndani katika mwaka huu wa fedha imeweza kumalizia maboma **28** ya Sekondari, kuendeleza ujenzi wa vyumba **15** katika shule mpya ya Sayansi ya Sekondari Boma na kukarabati mmomonyoko wa udongo, mifereji ya maji ya mvua na gati katika shule ya Sekondari ya Bungodimwe ambapo gharama yake ni **Tshs 687,421,270.00** .

**Jedwali hapa chini linaonesha mgawanyo wa fedha uliofanyika.**

| JINA LA MRADI | HALI YA KAZI | KIASI |
|---|---|---|
| Umaliziaji wa maboma 2 ya madarasa katika shule ya sekondari Kingo | Imekamilika | 32,888,500 |
| Umaliziaji wa maboma 2 ya madarasa katika shule ya sekondari Mbuyuni | Imekamilika | 32,888,500 |
| Umaliziaji wa maboma 3 ya madarasa katika shule ya sekondari Tungi | Imekamilika | 48,434,000 |
| Umaliziaji wa maboma 3 ya madarasa katika shule ya sekondari Lukobe | Imekamilika | 49,625,000 |
| Umaliziaji wa madarasa 6 katika shule ya sekondari Mkundi | Hatua ya ukamilishaji | 29,500,000 |
| Umaliziaji wa madarasa 3 katika shule ya sekondari Mindu | Hatua ya ukamilishaji | 10,770,160 |

| | | |
|---|---|---|
| Umaliziaji wa maboma 3 ya madarasa katika shule ya sekondari Mafiga | Hatua ya ukamilishaji | 56,205,400 |
| Umaliziaji wa maboma 2 ya madarasa katika shule ya sekondari Bondwa | Hatua ya ukamilishaji | 37,503,410 |
| Umaliziaji wa maboma 2 ya madarasa na ofisi katika shule ya sekondari Mazimbu | Hatua ya ukamilishaji | 23,637,500 |
| Uendelezaji wa ujenzi wa shule ya Ghorofa Boma yenye vyumba 15 | Hatua ya uendelezaji | 362,952,960 |
| Kukarabati mmomonyoko wa udongo, mifereji ya maji ya mvua | mekamilika | 3,015,840 |
| **JUMLA KUU** | | **687,421,270.00** |

Aidha, Manispaa imejenga matundu **52** ya vyoo katika shule mpya **4** na kongwe **1** yaani Shule za sekondari ya Kola Hill matundu **10**, Mazimbu matundu **10**, Mbuyuni matundu **10**, Tungi matundu **10** na Mkundi matundu **12** ambapo matundu **10** ya Wanafunzi na matundu **2** ya Walimu jumla ya **Tshs. 40,000,000.00** zimetumika.

**Mchanganuo wa ujenzi wa matundu ya vyoo.**

| SN | JINA LA MRADI | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Kola Hill-Kongwe | 7,000,000.00 | Ujenzi umekamilika |
| 2 | Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Mazimbu.-Mpya | 7,000,000.00 | Ujenzi umekamilika |
| 3 | Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Mbuyuni.-Mpya | 7,000,000.00 | Ujenzi umekamilika |
| 4 | Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Tungi.-Mpya | 7,000,000.00 | Ujenzi umekamilika |
| 5 | Ujenzi wa matundu 12 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Mkundi.-Mpya | 12,000,000.00 | Ujenzi umekamilika |
| | **JUMLA** | **40,000,000.00** | |

## ii) SEKTA YA ELIMU MSINGI

- Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2021/22 imekamilisha ujenzi wa vyumba **2** vya madarasa katika shule ya msingi Kilongo Kata ya Kihonda kwa **Tshs. 31,370,000.00**
- Manispaa imetenga jumla ya **Tshs 80,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya **8** na Ofisi **1** katika shule ya msingi Kilakala Kata ya Kilakala. Ujenzi wake unaendelea upo hatua za kumalizia.
- Manispaa imelipa jumla ya **Tshs 34,996,743.00** kama mchango wa mradi wa ujenzi wa uzio wa shule ya Msingi Kingolwira. Mradi huo umetekelezwa kwa msaada ya Shirika la Msaada la kimataifa la Japan (JICA) kwa makubaliano ya Manispaa kulipia VAT asilimia **18** ya mradi wa ujenzi huo.

## iii) SEKTA YA AFYA.

Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2021/22 imepeleka jumla ya **Tshs. 424,554,891.50** kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Zahanati **9** ndani ya Manispaa.

Zahanati **6** zimekamilika kabisa ambazo ni Tungi, Kihonda Maghorofani, Mbuyuni, Mgaza-Mindu, Sultan Area, K/Ndege na zahanati **3** zipo katika hatua mbalimbali za umaliziaji.

**Jedwali hapa chini linaonesha mgawanyo wa fedha uliofanyika.**

| S/N | JINA LA MRADI | HALI YA KAZI | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Umaliziaji wa zahanati ya Mbuyuni | Kazi inaendelea | 84,593,928.50 |
| 2 | Umaliziaji wa zahanati ya Mgaza/Mindu | Kazi inaendelea | 35,608,330.00 |
| 3 | Umaliziaji wa zahanati ya Sultan Area | Kazi inaendelea | 34,174,030.00 |
| 4 | Umaliziaji wa zahanati ya K/Ndege | Kazi inaendelea | 70,178,603.00 |
| 5 | Umaliziaji wa zahanati ya Tungi | Imekamilika | 0 |
| 6 | Umaliziaji wa zahanati ya Kihonda Maghorofani | Imekamilika | 30,000,000.00 |
| 7 | **Kumalizia Ujenzi wa Zahanati ya Mazimbu** | Kazi inaendelea | **100,000,000.00** |
| 8 | Kuendeleza ujenzi wa zahanati ya Uwanja wa Taifa | Kazi inaendelea | 20,000,000.00 |
| 9 | Kuanzisha ujenzi wa zahanati ya Kauzeni | Mchakato wa kazi za ujenzi unaendelea | 50,000,000.00 |
| | **JUMLA** | | **424,554,891.50** |

Aidha, Manispaa kwa kutumia fedha zake za ndani imeanzisha ujenzi wa majengo 10 ya kituo cha Afya Tungi ambapo inakadiriwa kutumia jumla ya **Tshs 350,000,000.00** ambazo zinaendelea na ujenzi. Kituo hiki kinatarajia kutumia takribani **Tshs 1,200,000,000.00** hadi kukamilika kwake. Huu ni mradi mkubwa sana wa afya ambao Manispaa imepania kuujenga kwa fedha zake yenyewe.

**iv) SEKTA YA MIPANGO MIJI, ARDHI NA MALIASILI**

Manispaa ya Morogoro katika jukumu lake la upangaji, upimaji, uthamini wa Ardhi, umilikishwaji wa Ardhi na usimamizi wa maendelezo ya Miji imetumia jumla ya **Tshs 127,670,000.00** kwa ajili ya maandalizi ya michoro, utambuzi wa eneo na umiliki wa wananchi pamoja na kufanya vikao vya wadau. Lengo kuu ni maandalizi ya kupima viwanja na kutoa hati za Ardhi katika maeneo ya Kiegea **A** na **B** yenye eneo la ekari **4,500**.

**(vi) MPANGO WA UTAMBUZI WA ANWANI ZA MAKAZI**

Manispaa ya Morogoro kwa kutambua umuhimu wa Anwani za Makazi na Postikodi kupitia mapato yake ya ndani imetoa kiasi cha **Tshs 200,000,000.00** kwa ajili ya shughuli za uandikishaji wa Anwani za makazi kwa lengo la kurahisisha mawasiliano, ufikishaji wa huduma za Serikali kwa wananchi na kufanyika kwa shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutawala. Hivyo ni utekelezaji wa Sera ya Posta ya mwaka 2003 inayotaka nchi kuwa na Anwani za Kitaifa kwa ufikishaji huduma za kijamii na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025.

**(vii) FEDHA ZA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2021/22 imeweza kutoa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu yaani asilimia **10** kuwa ni **Tshs 631,150,000.00** ambapo Wanawake **Tshs 409,000,000.00**, Vijana **Tshs 186,000,000** na walemavu **Tshs 36,150,000.00**

**MIPANGO YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

Mbali na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri katika mwaka 2022/2023 imeweka vipaumbele katika maeneo sita ambayo ni;

i. Makusanyo ya Mapato
ii. Elimu
iii. Afya

iv. Usafi wa Mji na utunzaji wa Mazingira
v. Utawala Bora
vi. Mipango Miji

Katika Mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri inategemea kukusanya na kutumia jumla ya kiasi cha **Tsh. 86,760,328,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| Mapato ya Ndani ................................. | 12,654,400,000.00 |
| Mishahara......................................... | 64,422,956,000.00 |
| Matumizi mengineyo............................. | 1,164,169,000.00 |
| Miradi ya maendeleo............................. | 8,518,803,000.00 |

Aidha, miradi ifuatayo inategemewa kukamilishwa.

i. Kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu (4:4:2).
ii. Kumalizia ujenzi wa kituo cha Afya Tungi.
iii. Kumalizia miundombinu ya zahanati 4 za Mji Mkuu, Kauzeni, Mafiga na Kihonda.
iv. Kumalizia ujenzi wa maboma 50 ya madarasa ya Shule za Msingi.
v. Kujenga matundu 20 ya vyoo katika Shule za Msingi Mbete na Towelo katika Kata ya Mlimani.
vi. Ujenzi wa majengo ya utawala katika Shule za Sekondari 7 za Mbuyuni, Tungi, Mazimbu, Mkundi, Kola Hill, Mafiga na Mwembesongo.
vii. Kuendeleza ujenzi wa shule ya sekondari Boma.
viii. Kununua mashine 150 za kukusanyia mapato na karatasi zake (PoS).
ix. Kukarabati miundombinu ya masoko mawili ya Mawenzi na Mjimpya.
x. Kununua magari 2 ya Idara ya Mipango Miji na Utawala (Pickup & Coaster).
xi. Ufungaji wa mifumo ya umwagiliaji kwenye kitalu nyumba katika Kata 5.
xii. Kununua mapipa 30 yenye ujazo wa kati kwa ajili ya kukusanyia taka.
xiii. Kujenga mifumo ya maji taka na kuunganisha katika mfumo mkuu (Soko la Mawenzi, Stendi ya Kaloleni na Stendi ya Mafiga).
xiv. Kuanzisha mradi wa vitalu vya miti.
xv. Kukarabati vifaa vya mtandao (network switch) jengo la utawala Manispaa (HQ).

xvi. Kugharamia shughuli za anuani za makazi (Postcode)
xvii. Kufungua barabara za Kata na Mitaa kwa kushirikiana na TARURA.
xviii. Kujaza kifusi/changarawe, kusawazisha na kushindilia eneo la mradi wa maegesho ya malori Nanenane.
xix. Kulipa fidia kwenye maeneo yanayopitiwa na miradi ya World Bank (TACTIC).
xx. Kuanzisha mradi wa kufyatua matofali.
xxi. Kufunga mfumo mpya wa umeme kwenye jengo la Manispaa (HQ).
xxii. Kununua jenerata kwa ajili ya ofisi za Manispaa (HQ).
xxiii. Kuboresha miundombinu ya Wafanyabiashara ndogondogo (Machinga).
xxiv. Kutekeleza miradi na shughuli za majanga.
xxv. Kuanzisha ujenzi wa ukumbi wa kisasa eneo la Manzese.
xxvi. Ujenzi wa njia ya watu wenye ulemavu (rump), uzio na kuweka vigae (paving) kitega uchumi cha Mbaraka Mwinshehe (DDC).
xxvii. Kugharamia maandiko ya miradi ya kimkakati.

## 3.0 SEKTA YA UJENZI

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Ujenzi ilijikita katika kuboresha miradi mbalimbali katika sekta ya Elimu, Afya na Utawala kama ifuatavyo:-

**i) Sekta ya Afya**:

- Ukamilishaji wa zahanati **Tano** (**5**) katika Kata ya Mbuyuni, Sultani Area, Mindu na Kiwanja cha Ndege.
- Ujenzi wa Vituo vya Afya Viwili (2) katika Kata ya Lukobe na Tungi
- Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kata ya Kihonda

**ii) Sekta ya Elimu**:

- Ukamilishaji wa vyumba **9** vya madarasa katika Shule za Sekondari.
- Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Kata ya Boma
- Ujenzi wa bweni la wanafunzi maalum katika shule ya msingi Kihonda (Noto)
- Ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Lukobe na Mindu
- Umaliziaji wa maabara Nne (**4**) katika shule za sekondari SUA, Kingalu, Mgulasi na Tushikamane.

- Umaliziaji wa ujenzi wa vyoo matundu Ishirini (**20**) shule ya sekondari SUA.

**iii) Utawala**:

- Ujenzi wa mabanda ya wamachinga eneo la soko la Fire na Mtaa wa Mindu Masika

## 4.0 KUHUSU SEKTA YA ELIMU YA MSINGI:

Halmashauri imefanikiwa kuongeza idadi ya Wanafunzi walioandikishwa kuanza darasa la awali na darasa la kwanza.

- **Darasa la awali**
  Wanafunzi waliosajiliwa kuingia darasa la awali mwaka 2022 ni **7,202**, wavulana **3,678** na wasichana **3,524** kwa shule za serikali na binafsi.

- **Darasa la kwanza**
  Wanafunzi waliosajiliwa kuingia darasa la kwanza mwaka 2022 ni **11,665** kati yao wavulana **5,829** na wasichana **5,836** kwa shule za serikali na binafsi

- **Mafanikio ya Sekta ya Elimu Msingi:**
  Kumekuwa na ongezeko la miundombinu ikiwemo madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na samani katika shule za msingi kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano madarasa yaliyopo ni **656** na mahitaji ni madarasa **1,539** hadi Juni, 2022.

  Aidha nyumba za walimu zilizopo ni **81** kati ya nyumba **2,074** zinazohitajika Juni, 2022. Pia matundu ya vyoo vya wanafunzi yaliyopo ni **729** ilipofika Juni 2022 na madawati mahitaji ni **2,173** na yaliyopo ni **14,230** ilipofika Juni 2022.

  Kwa upande wa vitabu uwiano kwa wanafunzi umepungua kutoka **1:3** mwaka 2022 hadi **1:2** ilipofika Juni 2022. Hali ya vitabu kwa sasa mashuleni kuanzia darasa la I – V inaridhisha. Halmashauri imepata vitabu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

- **Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi**
  Waheshimiwa Madiwani Mwaka 2021 mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ulifanyika mwezi Septemba, 2021. Jumla ya watahiniwa **8,852** walisajiliwa ambapo wavulana **4,392** na wasichana **4,460**.

Ufaulu wa wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka 2021 ulikuwa ni **asilimia 94.2,** wanafunzi **8,292** walifaulu wakiwemo wavulana **4,054** na wasichana **4,238** kati ya **8,802** waliofanya mtihani wakiwemo wavulana **4,362** na wasichana **4,440** jumla **8,802**.

| | **MAHITAJI** | **YALIYOPO** | **UPUNGUFU** |
|---|---|---|---|
| Awali | 3,586 | 723 | 2,686 |
| Msingi (I – VII) | 20,570 | 14,477 | 6,093 |
| **JUMLA** | **23,979** | **15,200** | **8,779** |

## 5.0 KUHUSU SEKTA YA ELIMU SEKONDARI.

Halmashauri ina jumla ya Shule **55**, kati ya hizo **27** ni za Serikali na **28** ni za binafsi. Wanafunzi **34,179** wakiwemo wavulana **16,513** na wasichana **17,666** kati ya Wanafunzi hao, Wanafunzi **24,408** ni wa Shule za Sekondari za Serikali, wakiwemo wavulana **11,937** na wasichana **13,471** na wanafunzi **8,771** ni wa shule za binafsi wakiwemo wavulana **4,576** na wasichana **4,195.**

**a) Taaluma**

Ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita mwaka **2021** ni asilimia **99.6** na **99.6** Juni, 2022. Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne imeongezeka kufikia asilimia **87** mwaka 2021.

**i) Mikakati ya kukabiliana na changamoto katika elimu ya Sekondari.**

Kuendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka ili kujenga na kukarabati miundombinu na samani za shule mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa.Kuwajengea uwezo walimu ili kuinua kiwango cha ufaulu na kuhakikisha tunafuta sifuri. Pia kuwapatia vitabu vya ziada na kiada walimu na wanafunzi, ukamilishaji waa vyumba vya maabara ili kuwahamasisha wanafunzi kupenda masomo ya Sayansi.

## 6.0 KUHUSU SEKTA YA AFYA

Shughuli zifuatazo zimefanyika katika Sekta ya Afya:-

i) Wigo wa dawa zinazopatikana vituoni umeongezeka kutoka asilimia **93.1** mwaka 2020/2021 mpaka kufikia asilimia **96**.8 mwaka 2021/2022, pia chanjo mbalimbali zinatolewa vituoni ikiwemo chanjo ya kichaa cha mbwa .

ii) Halmashauri imefanikisha ujenzi wa zahanati 6 ambazo ni Kihonda Magorofani, Mganza, Tungi, Sultan Area, Kiwanja cha Ndege na Mbuyuni. Hivyo kufanya jumla ya vituo vya kutolea huduma ya Afya vya Serikali kuongezeka kutoka vituo 22 mwaka 2020/2021 kufikia 28 mwaka 2021/2022.

iii) Pia Halmashauri imefanikisha ununuzi wa samani kwenye vituo vipya zikiwemo meza 24, Viti 24, benchi 24 na kabati za kuwekea dawa 6 vikiwa na thamani ya **Tsh Mil 10.**

iv) Aidha Halmashauri inaendelea na ujenzi wa kituo cha Afya Lukobe na Tungi ambapo majengo mbalimbali yamefikia hatua ya linta ikiwemo jengo la upasuaji, jengo la wagonjwa wa kulazwa, jengo la Xray, jengo la kuhifadhi maiti, jengo la kufulia, jengo la wazazi, maabara, kichomea taka na jengo la watumishi.

v) Kufanikisha kufunga mfumo wa "Got homis" katika zahanati 4 za kutolea huduma ya Afya ambazo ni Mwembesongo, Malipula, Misongeni na Kilakala lengo likiwa ni kusimamia makusanyo ya mapato ya vituo na taarifa za wateja kwa ujumla. Aidha Halmashauri inaendelea kufunga mfumo kwenye vituo vilivyabaki.

## 7.0 SEKTA YA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU

Shughuli za usafi na uhifadhi wa mazingira katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 zimeendelea kuboreshwa kwa kufanya yafuatayo:-

i) Kubinafsisha shughuli za usafi wa mazingira kwa Kampuni moja kuhudumia Kata **12** na vikundi **13** kuhudumia Kata **14.**

ii) Kubinafsisha usafi wa masoko ya Chifu Kingalu, Mawenzi na Mjimpya kwa Kampuni ya usafi.

iii) Kuweka utaratibu kwa Wazabuni wa kuzoa taka kukodi magari ya Manispaa.

iv) Kubinafsisha huduma ya utunzaji wa bustani na mizunguko ya barabara kwa Mzabuni.

v) Kubinafsisha huduma ya kusafisha barabara na mifereji ya maji ya mvua. Barabara zilizobinafsishwa zina urefu wa kilometa 51.9.

vi) Barabara za katikati ya mji zenye urefu wa kilometa 4 kufanyiwa usafi wa Kampuni ya usafi.

vii) Kufanya mapitio ya ada ya uzoaji wa taka ili zikidhi gharama za usafi.

## 8.0 KUHUSU UTAWALA BORA:

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imeendelea kusimamia matumizi ya misingi ya utawala bora ambao ni utawala wa kidemokrasia, ushirikishwaji wa umma, utawala wa kisheria, haki na usawa kwa watu wote, uwazi katika kuendesha shughuli za maendeleo, uwajibikaji katika utendaji na uadilifu.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imeshuhudia kuongezeka kwa uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma, kupungua kwa malalamiko yanayohusiana na utoaji huduma, vikao na mikutano kuendeshwa kwa mujibu wa ratiba na kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi katika mikutano hiyo.

### i) Upandishaji vyeo Watumishi

Baada ya Serikali ya awamu ya sita kuidhinisha upandishaji vyeo watumishi nchini, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 949 kwa mchanganuo ufuatao:_

- Idara ya Elimu Msingi ni 647
- Idara ya Elimu Sekondari 239
- Idara ya Afya 43
- Watumishi wengine 20

**Jumla 949**

## 9.0 SEKTA YA MAENDELEO Y A JAMII

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri imetoa mikopo yenye thamani ya **Tshs. 631,150,000.00** kwa vikundi **60** ambapo kiasi cha **Tshs. 409,000,000.00** kwa vikundi **39** vya Wanawake na **Tshs. 186,000,000.00** kwa vikundi **16** vya vijana na **Tshs. 36,150,000.00** kwa vikundi **05** vya wenye Ulemavu.

Idara imeendelea kuhamasisha uundaji na usajili wa vikundi ambapo Jumla ya vikundi **453** vya huduma ndogo ya kifedha vimesajiliwa. Pia vikundi **379** vya kijamii vimepata usajili hivyo kufanya vikundi vilivyosajiliwa kuwa **832.**

Idara imeweza kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa Jamii ulioboreshwa ambapo jumla ya Kaya **2,230**, zenye wanufaika **11,540** zimeandikishwa na kuingiza kiasi cha **Tshs. 66,900,000.00**.

## 10.0 MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF III(II)

Manispaa ni miongoni mwa Halmashauri **186** zinazotekeleza TASAF awamu ya tatu sehemu ya pili kupitia Mpango wa kunusuru Kaya maskini, wenye malengo ya kuwezesha kaya za walengwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za jamii na kuwekeza katika kuendeleza watoto wao pia kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na msisitizo mkubwa ukiwa katika mambo yafuatayo:-

i) Kuwezesha kaya kufanya kazi na kuongeza kipato;
ii) Kuwezesha kaya za walengwa kuongeza rasilimali zalishi na kuongeza vitega uchumi;
iii) Kuwekeza katika watoto ili kuleta matokeo chanya yatakayodumu kwa muda mrefu;
iv) Kuboresha upatikanaji wa huduma za maji, afya na elimu;
v) Kukuza uchumi wa eneo unakofanyika utekelezaji kutokana na matokeo ya Mpango.

Kuanzia Julai 2021 hadi Juni, 2022 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina jumla ya walengwa **3,607** kutoka katika Mitaa **258** kwa Kata zote **29** inayotekeleza mpango wa kunusuru Kaya masikini (TASAF III).

**Uhawilishaji fedha kwa Kaya Maskin**i **Mafanikio:-**

i) Kupitia Mpango wa TASAF kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Manispaa ya Morogoro ilipokea jumla ya shilingi **744,677,933.00** kutoka TASAF makao makuu na kufanya uhawilishaji kwa Walengwa wa kaya Maskini **3,604** moja kwa moja haya ni malipo ya vipindi vitano tu vya malipo (Julai/Agosti, 2021 - Machi/Aprili, 2022).

ii) Walengwa wa Mpango wameweza kukuza kipato cha familia na kuwa na uwezo wa kupata milo mitatu kwa siku Walengwa **1,937** waliotembelewa walithibitisha.

iii) Walengwa **137** toka mitaa mbalimbali ya mpango walihojiwa kupitia ruzuku wameweza kupata fedha ambazo zinawasaidia kulima mashamba ya mahindi na Alizeti.

iv) Kupitia ruzuku hii kuna walengwa takribani **2001** sawa na asilimia **56** wameweza kuanzisha biashara ndogo ndogo za kuuza ndizi, magenge, ufugaji wa mifugo kama Mbuzi, Nguruwe n.k.

v) Walengwa **1,602** (me **39** na ke **1,602**) wameweza kuunda vikundi **132** na kujiwekea akiba ya **Tsh.21,810,800.00** kupitia utaratibu wa kuweka na kuwekeza na wanakopeshana wao kwa wao, hivyo wameweza kukuza uchumi wa kaya kwa kuendesha miradi/biashara ndogondogo.

vi) Pia Walengwa wameweza Kuongeza uwezo wa kuhudumia mahitaji ya shule kwa watoto wao kama madaftari, sare za shule na mahitaji mengine ya msingi

HMM/BM/2/2022/2023 Kuridhia Agenda za Mkutano

Baraza la Madiwani liliridhia agenda zifuatazo:-

1. Kufungua Mkutano.
2. Kumchagua Naibu Meya wa Manispaa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.
3. Kuteua Wajumbe wa Kamati za Kudumu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.
4. Kujadili taarifa ya utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri kwa mwaka 2021/2022.
5. Kupitisha ratiba ya vkao vya Halmashsuri na Kamati za Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.
6. Kufunga Mkutano.

HMM/BM/3/2022/2023 Kumchagua Naibu Meya wa Manispaa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) alieleza kuwa alimuandikia barua Katibu wa CCM Wilaya yenye kumb. Na.A30/MMC-237/78 ya tarehe 13/6/2022 ili afanye uchaguzi wa jina la Naibu Meya wa Manispaa wa mwaka wa fedha 2022/2023 na kuliwasilisha kabla ya tarehe 30/6/2022 ili kufanya uchaguzi. Katibu wa CCM Wilaya aliandika barua kwa Mkurugenzi wa Manispaa yenye Kumb. Na.CCM/W/MG/Vol.3/158/24 ya tarehe 14/07/2022 ikimtambulisha Mheshimiwa Mohamed Yahaya Lukwele kuwa Naibu Meya wa Manispaa kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

Kwa kuwa Baraza la Madiwani la Manispaa ya Morogoro linaundwa na Waheshimiwa Madiwani wa Chama kimoja cha CCM na kwa kuzingatia Kanuni ya kudumu ya Halmashsuri ya Manispaa ya Morogoro Namba 10 (4), Wajumbe walitangaziwa kuwa ikiwa kutakuwa na jina moja la mgombea zitapigiwa kura za siri za "ndiyo" au "hapana" na endapo kura za ndiyo zitazidi asilimia hamsini ya kura zote zilizopigwa basi mgombea atatangazwa kuwa mshindi.

Kabla ya uchaguzi Mheshimiwa Mohamed Yahaya Lukwele Naibu Meya aliyemaliza muda wake aliwashukuru Wajumbe na Wataalamu kwa kumpa ushirikiano katika kipindi chote alichokuwa madarakani. Aidha, aliwaomba Wajumbe kumpa kura zote za ndiyo katika uchaguzi wa nafasi ya Naibu Meya kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Baada ya kusema hayo Naibu Meya aliemaliza muda wake alijiuzuru ili kupisha uchaguzi.

**Utaratibu wa uchaguzi wa Naibu Meya wa Manispaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.** Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) alimteua Ndugu Samwel Tyeah- Mwanasheria wa Manispaa kuwa msimamizi wa uchaguzi wa Naibu Meya wa Manispaa ya Morogoro. Wajumbe walipiga kura za siri na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-
Wajumbe waliopiga kura…..38
Kura zilizoharibika……………..0
Kura za hapana …………………0
Kura halali za ndiyo…………..38
Kwa mamlaka aliyopewa, Mwanasheria wa Manispaa alimtangaza Mheshimiwa Mohamed Yahaya Lukwele kuwa Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023. Naibu Meya aliwashukuru Wajumbe kwa kumpa kura za ndiyo kwa asilimia 100.

HMM/BM/4/2022/2023 Kuteua Wajumbe wa Kamati za Kudumu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Mstahiki Meya aliwaomba Wajumbe waridhie kuvunja Kamati ya Bodi ya Ngozi kwa kuwa haipo hai pia aliomba idhini ya kuunda Kamati Ndogo ya Afya ili kusimamisha masuala ya Zahanati na Vituo vya Afya vya Manispaa. Wajumbe wa Baraza la Madiwani waliridhia maombi hayo. Kabla ya kuunda Kamati Wenyeviti wa Kamati za Huduma za Uchumi, Eimu na Afya, Mipango miji na Mazingira, na Maadili ya Madiwani walijiuzuru kwa niaba ya Kamati zao. Kwa mamlaka aliyopewa, Mstahiki Meya aliunda Kamati za Kudumu, Kamati Ndogo na Kamati nyingine na Baraza iliridhia. Kamati ziliundwa kama ifuatayo:-

1. **KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI.**

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| 1) | Mhe. Pascal M. Kihanga | Mstahiki Meya - Mwenyekiti |
| 2) | Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele | Naibu Meya - Mjumbe |
| 3) | Mhe. Abdulaziz Mohamed (MB) | Mjumbe |
| 4) | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | Mjumbe |
| 5) | Mhe. Amini Abdallah Tunda | Mjumbe |
| 6) | Mhe. Zamoyoni J. Abdallah | Mjumbe |
| 7) | Mhe. Salma Bonzo Mbandu | Mjumbe |
| 8) | Mhe. Latifa Ganzel | Mjumbe |
| 9) | Mhe. Peter Joel Dhahabu | Mjumbe |
| 10) | Mhe. Selestini Savin Mbilinyi | Mjumbe |
| 11) | Mhe. Eng. Hamis Hamad Ndwata | Mjumbe |

**2. KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI, ELIMU NA AFYA:**

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Amini Abdallah Tunda | Mwenyekiti |
| 2 | Mhe. Pascal M. Kihanga | Mstahiki Meya – Mjumbe |
| 3 | Mhe. Dr. Christine Ishengoma(Mb) | Mjumbe |
| 4 | Mhe. Abdallah Ally Meya | Mjumbe |
| 5 | Mhe. Thomas Benedict Butabile | Mjumbe |
| 6 | Mhe. Melichior Peter Mwamnyanyi | Mjumbe |
| 7 | Mhe. Zuber George Mkalaboko | Mjumbe |
| 8 | Mhe. Selestini Savin Mbilinyi | Mjumbe |
| 9 | Mhe. Emmy Kiula Rajabu | Mjumbe |
| 10 | Mhe. Namala Johaness Mchunguzi | Mjumbe |
| 11 | Mhe. Hassan Madadi Maringo | Mjumbe |
| 12 | Mhe. Peter Joel Dhahabu | Mjumbe |
| 13 | Mhe. Rahma Lashayo Maumba | Mjumbe |
| 14 | Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani | Mjumbe |
| 15 | Mhe. Marco Mathias Kanga | Mjumbe |
| 16 | Mhe. Zamoyoni J. Abdallah | Mjumbe |
| 17 | Mhe. Amina H. Zihuye | Mjumbe |
| 18 | Mhe. Mwanaidi E. Ngulungu | Mjumbe |
| 19 | Mhe. Aisha Ahmad Kitime | Mjumbe |
| 20 | Mhe. Lt. Col. (Mst) Ahmed Salum Mazora | Mjumbe |
| 21 | Mhe. Rashid Ramadhani Matessa | Mjumbe |

**3. KAMATI YA MIPANGOMIJI NA MAZINGIRA**:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | Mwenyekiti |
| 2 | Mhe. Pascal M. Kihanga | Mstahiki Meya – Mjumbe |
| 3 | Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood (Mb) | Mjumbe |
| 4 | Mhe. Norah Mzeru (Mb) | Mjumbe |
| 5 | Mhe. Hamisi Ally Kilongo | Mjumbe |
| 6 | Mhe. Salum Mrisho Chunga | Mjumbe |
| 7 | Mhe. Samwel Msuya | Mjumbe |
| 8 | Mhe. Seif Zahoro Chomoka | Mjumbe |
| 9 | Mhe. Zinduna Kombo Selemani | Mjumbe |
| 10 | Mhe. Eng. Hamis Hamad Ndwata | Mjumbe |
| 11 | Mhe. Madaraka Steven Bidyanguze | Mjumbe |
| 12 | Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu | Mjumbe |
| 13 | Mhe. Juma Issa Kiduka | Mjumbe |
| 14 | Mhe. Athuman Omary Lujuo | Mjumbe |
| 15 | Mhe. Warda O. Bazia | Mjumbe |
| 16 | Mhe. Joel Albart Kisome | Mjumbe |
| 17 | Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu | Mjumbe |
| 18 | Mhe. Hadija K. Kibati | Mjumbe |
| 19 | Mhe. Salima Bonzo Mbandu | Mjumbe |
| 20 | Mhe. Grace L. Mkumbae | Mjumbe |
| 21 | Mhe. Latifa Said Ganzel | Mjumbe |

## 4. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| | Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele | Naibu Meya - Mwenyekiti |
| | Mhe. Pascal M. Kihanga | Mstahiki Meya - Mjumbe |
| | Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb) | Mjumbe |
| | Mhe. Norah Mzeru (Mb) | Mjumbe |
| | Mhe. Dr. Christine Ishengoma (Mb) | Mjumbe |
| | Mhe. Marco Mathias Kanga | Mjumbe |
| | Mhe. Mwanaidi E. Ngulungu | Mjumbe |
| | Mhe. Amina H. Zihuye | Mjumbe |
| | Mhe. Zuberi Gerge Mkalaboko | Mjumbe |

## 5. KAMATI YA MAADILI:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| | Mhe. Madaraka Steven Bidyanguze | Mwenyekiti |
| | Mhe. Emmy Kiula Rajabu | Mjumbe |
| | Mhe. Melichior Peter Mwamnyanyi | Mjumbe |
| | Mhe. Thomas Benedict Butabile | Mjumbe |
| | Mhe. Zinduna Kombo Sulemani | Mjumbe |
| | Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu | Mjumbe |

**6. KAMATI NDOGO YA MAZINGIRA**

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| 1) | Mhe. Hamisi Ally Kilongo | Mwenyekiti |
| 2) | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | Mjumbe |
| 3) | Mhe. Joel Albart Kisome | Mjumbe |
| 4) | Mhe. Samwel A. Msuya | Mjumbe |
| 5) | Mhe. Grace L. Mkumbae | Mjumbe |
| 6) | Mhe. Athuman Omary Lujuo | Mjumbe |

**7. KAMATI YA NDOGO YA AFYA**:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| | Mhe. Aisha Ahamadi Kitime | Mwenyekiti |
| | Mhe. Amini Abdallah Tunda | Mjumbe |
| | Mhe. Hassan Madadi Maringo | Mjumbe |
| | Mhe. Namala Johanes Mchunguzi | Mjumbe |
| | Mhe. Abdallah Ally Meya | Mjumbe |
| | Mhe. Rashid Ramadhani Matessa | Mjumbe |

**8. KAMATI YA KUGAWA ARDHI**:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| | Mhe. Juma Issa Kiduka | Mjumbe |
| | Mhe. Warda O. Bazia | Mjumbe |

**9. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA AGM MSAMVU PROPERTIES**:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| | Mhe. Pascal M. Kihanga | Mstahiki Meya |
| 2) | Mhe. Seif Zahoro Chomoka | Mjumbe |

**10. MFUKO WA JIMBO**:

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| | Mhe. Abdul Aziz Mohamed (Mb) | Mwenyekiti |
| | Mhe. Rahma Lashayo Maumba | Mjumbe |
| | Mhe. Salum Mrisho Chunga | Mjumbe |
| | Ndg. Bright Sospeter | WEO - Mjumbe |
| | Ndg. Prisca C. Mawallah | WEO - Mjumbe |

**11. ALAT MKOA**

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| 1) | Mhe. Pascal M. Kihanga | Mstahiki Meya |
| 2) | Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb) | Mjumbe |
| 3) | Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani | Mjumbe |
| 4) | Mhe. Hadija K. Kibati | Mjumbe |

**12. BODI YA AJIRA**

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| 1) | Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu | Mjumbe |

**13. BODI YA MORUWASA**

| NA | JINA KAMILI | NAFASI |
|---|---|---|
| **1)** | Mhe. Lt. Col. (Mst) Ahmed Salum Mazora | Mjumbe |

Aidha demokrasia iitumika katika kuwachagua Wenyeviti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya, Mipangomiji na Mazingira Maadili ya Madiwani, Kamati Ndogo ya Afya na Kamati Ndogo ya Mazingira.

HMM/BM/5/ 2022/2023 Kujadili taarifa ya utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

| | |
|---|---|
| HMM/BM/6/ 2022/2023<br>Kupitisha ratiba ya vikao vya Halmashsuri na kamati za Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. | Baraza la Madiwani lilipokea na kuridhia ratiba ya vikao vya Halmashauri na Kamati zake kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:- |

**i) KAMATI ZA KUDUMU KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023**

| NA. | KAMATI | 2022 | | | | | | 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | JUL | AUG | SEP | OKT | NOV | DES | JAN | FEB | MACHI | APR | MEI | JUNI |
| 1) | Fedha na Uongozi | | 3 ziara<br>4 kikao<br>24 ziara<br>25 kikao | 20 | 19 ziara<br>20 kikao | 17 | 20 | 18 ziara<br>19 kikao | 16 | 16 | 19 ziara<br>20 kikao | 18 | 20 |
| 2) | Huduma za Uchumi, Elimu na Afya | 25 ziara<br>26kikao | | | 10 ziara<br>11 kikao | | | 05 ziara<br>06 kikao | | | 5 ziara<br>6 kikao | | |
| 3) | Mipangomiji na Mazingira | 27ziara<br>28 kikao | | | 12 ziara<br>13 kikao | | | 09 ziara<br>10 kikao | | | 11 ziara<br>12 kikao | | |
| 4) | Kudhibiti UKIMWI | 29 ziara<br>29 kikao | | | 17 ziara<br>17 kikao | | | 11 ziara<br>11 kikao | | | 14 ziara<br>14 kikao | | |
| 5) | Maadili ya Madiwani | | 5 | | 20 | | | 18 | | | 20 | | |
| 6) | Bodi ya Huduma za Afya | 25 | | | 28 | | | 23 | | | 21 | | |
| 7) | Uwasilishaji wa taarifa za Kata (Madiwani) | | 9 | | 25 | | | 26 | | | 24 | | |
| 8) | Kamati za Vyama Madiwani | | 10 | | 26 | | | 30 | | | 25 | | |
| 9) | Baraza la Madiwani | | 11 | | 27 | | | 31 | | | 27 | | 30 |
| 10) | *Kamati ya Ushauri Wilaya | | | | | | | | | | | | |
| 11) | Kamati ya Wataalamu wa Halmashauri | 15 | 22 | 12 | 05 | 10 | 13 | 3 | 9 | 10 | 4 | 11 | 13 |
| 12) | Baraza la Wafanyakazi | | | | | 25 | | | | | | | 28 |
| 13) | Bodi ya Zabuni | 08 | | | 28 | | | 28 | | | 28 | | |

### ii) KAMATI NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023

| NA. | KAMATI | 2022 | | | | | | 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | JUL | AUG | SEP | OKT | NOV | DES | JAN | FEB | MACHI | APR | MEI | JUNI |
| 1) | Vibali vya Ujenzi | 5 ziara<br>5 kikao<br>22 ziara<br>22 kikao | 9 ziara<br>9 kikao<br>22 ziara<br>22 kikao | 8 ziara<br>8 kikao<br>19 ziara<br>19 kikao | 6 ziara<br>6 kikao<br>19 ziara<br>19 kikao | 3 kikao<br>3 ziara<br>30 kikao<br>30 ziara | 2 ziara<br>2 kikao<br>23 ziara<br>23 kikao | 4 ziara<br>4 kikao<br>19 ziara<br>19 kikao | 6 ziara<br>6 kikao<br>24 ziara<br>24 kikao | 6 ziara<br>6 kikao<br>24 ziara<br>24 kikao | 6 ziara<br>6 kikao<br>25 ziara<br>25 kikao | 5 ziara<br>5 kikao<br>25 ziara<br>25 kikao | 2 ziara<br>2 kikao<br>26 ziara<br>26 kikao |
| 2) | * Kugawa Ardhi | | | | | | | | | | | | |
| 3) | * Uongozi wa Mradi wa Upimaji Viwanja 4,000 | | | | | | | | | | | | |
| 4) | Leseni za Vileo | | | 15 | | | | | | 16 | | | |
| 5) | Kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi | 8 | | | 7 | | | 5 | | | 6 | | |
| 6) | Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | 29 | | | | | | 28 | | | | | |
| 7) | Kamati ya Nyumba | 28 | | | 31 | | | 31 | | | 27 | | |
| 9) | *Bodi ya Ajira | *6 | | | *7 | | | *13 | | | *6 | | |
| 10) | Kamati ya Ukaguzi | 8 | | | 7 | | | 11 | | | 12 | | |
| 11) | Kamati Ndogo ya Mazingira | 11 ziara<br>11 kikao | | | | | | 2 ziara<br>2 kikao | | | 5 ziara<br>5 kikao | | |
| 12) | Kamati ya Mikopo ya Wilaya | 29 | | | 28 | | | 23 | | | 22 | | |
| 13) | Kamati ya Lishe | 29 | | | 21 | | | 27 | | | 29 | | |
| 14) | * Kamati ya Mfuko wa Jimbo | | | | | | | | | | | | |
| 15) | Kamati tendaji Baraza la Wafanyakazi | | | | | 18 | | | | | | | 23 |
| 16 | Kamati ya Mipangomiji ya Wataalam | 1 ziara<br>1 kikao | 24ziara<br>24 kikao | 29 ziara<br>29 kikao | 28 ziara<br>28 kikao | 29 ziara<br>29 kikao | 29 ziara<br>30kikao | 13 ziara<br>13 kikao | 24 ziara<br>24 kikao | 23 ziara<br>24 kikao | 28 ziara<br>28 kikao | 30 ziara<br>31 kikao | 27 ziara<br>28 kikao |
| 17 | Kamati Ndogo ya Afya | 22 | | | 6 | | | 4 | | | 3 | | |

| | |
|---|---|
| HMM/BM/7/ 2022/2023 Kufunga Mkutano | Kabla ya kufunga mkutano, Mstahiki Meya aliwakaribisha Viongozi wafuatao ili waongee na Wajumbe wa Baraza la Madiwani. |

**1. Katibu wa CCM Wilaya:-**

Alilipongeza Baraza la Madiwani na Wataalamu kwa kutoa taarifa nzuri ya utendaji yenye takwimu. Aidha aliipongeza Halmashauri kwa kufikisha zaidi ya asilimia 85 ya makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Alitoa pongezi kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kusimamia vizuri makusanyiko ya mapato ya Halmashauri hivyo kusimamia utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025. Alishauri Halmashauri ianzishe miradi ya kimkakati ili kuweza kufikia azma ya kuwa Jiji.

**Kuhusu mapipa ya taka:-**

Alishauri kuwa Halmashauri itengeneze mapipa ya taka ya kuhifadhia taka ngumu kwa kutumia chuma chakavu na yasambazwe Mitaani.

**2. Salaam za Katibu Tawala Wilaya:-**

Alilipongeza Baraza la Madiwani na Halmashauri kwa mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022.

**3. Salaam za Mkurugenzi wa Manispaa.**

Mkurugenzi wa Manispaa alikishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa kulisimamia vizuri Baraza la Madiwani na Wataalamu wa Halmashauri na kutoa ushauri na kuwaongoza katika utendaji na usimamizi ili kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya Halmashauri na utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025. Aidha aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Halmashauri kwa kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake na aliomba ushirikiano huo uendelee. Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa kufikisha asilimia zaidi ya 85 kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Utawala Bora, Usafi wa Mazingira, Mipangomiji na Afya ambapo Serikali Kuu imeleta watumishi **18** wa Afya kuhudumia zahanati 6 mpya za Manispaa.

Baada ya salaam hizo Mstahiki Meya aliwashukuru Wajumbe na Viongozi waliohudhuria mkutano na kutoa hoja mballimbali. Aidha aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge na Wataalamu wote kwa kumpa ushirikiano ili kufikia azma ya Halmashauri kuwa Jiji.

Baada ya kusema hayo, Mstahiki Meya alifunga mkutano saa 7:10 mchana.

Muhtasari umethibitishwa tarehe ……………………..…………………………

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| Mhe. Pascal M. Kihanga | Ndg. Ally H. Machela |
| MSTAHIKI MEYA | MKURUGENZI WA MANISPAA |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

## YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 28/04/2022

| MUHT. NA | AZIMIO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| HMM/BM/81/ 2021/2022 Kufungua Mkutano | **1.0 Kuhusu mikataba ya Wafanyabiashara eneo la Zimamoto**<br>Aliagiza kuwa mikataba **51** ya Wafanyabiashara eneo la Zimamoto ambayo haipo rasmi ifutwe na kuingiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na kulipa Mapato ya Halmashauri. | Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi (MS, MTO, MT) | |
| | **2.0 Kuhusu stendi ya Daladala Mafiga**<br>Aliagiza kuwa Stendi ya Daladala Mafiga ifanye kazi, magari yote yanayoenda Wilayani yaanzie hapo. | Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya (MD) | |
| | **3.0 Kuhusu wauza mbogamboga na matunda katikati ya mji**<br>Menejimenti iwasilishe mchanganuo wa fedha **Shs 200,000,000.00** za ujenzi wa mabanda ya Wafanyabiashara ndogo ndogo eneo la Zimamoto wenye kikao kijacho cha | Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi (ME) | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Fedha na Uongozi kisha kwenye mkutano ujao wa Baraza la Madiwani. | | |
| HMM/BM/86/ 2021/2022 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo | **4.0** | **Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.** Baraza la Madiwani lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa kuiandikia barua Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro (MORUWASA) ili iache kudai vibali vya ujenzi kwa nyumba zilizokwisha jengwa kuanzia mwaka 2015 kurudi nyuma. | Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya (ME) | |
| HMM/BM/89/ 2021/2022 Taarifa mbalimbali | **5.0** | **Kuhusu Stendi ya Daladala Mafiga** Baraza lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa, Wataalamu wa Manispaa na SUA waende katika stendi ya Daladala Mafiga kuangalia kama kilichofanyika pale kina tija kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na SUA na awasilishe taarifa kwenye Mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani. | Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi (MESO) | |